**ICC-PIDS-PR-250-Sw**

**Mtu wa pili kukamatiwa : Germain Katanga anapelekewa ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai**

La Haye, siku 18 mwezi ya kumi 2007

ICC-20071018-250-Sw

**Hali** : Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
**Afere :** Prokirere c. Germain Katanga

Siku 17 za mwezi ya kumi 2007, Germain Katanga, akiwa ni Mkongomani na mwenye banazania kama ni kiongozi wa *Force de résistance patriotique en Ituri (FRPI)* alipaniwa na serikali ya Kongo ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai na akabebewa ku makao makuu ya ile Mahakama. Akijulikana tena ku jina ya « Simba », anazaniwa kama alifanya jinai sita za vitani na jinai tatu dhidi ya utu pale Ituri mu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Masambo yenye kumuangalia iko ndani ya hali mu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, yenye biro ya Prokirere iko inafanya ako ankete tangu siku 1 mwezi ya saba 2002.

Siku yenye Germain Katanga atapita turu ya kwanza mbele ya tribinale itajulishwa nyuma.

**Maneno yenye kusemeka**

Siku 2 mwezi ya saba, kisha kujifunza ombi na ushahidi yenye Prokirere alileta, Chumba cha utangulizi I kilifanya manda ya kukamata Germain Katanga yenye kuwa na mhuri ya siri. Ile mhuri ya siri ilitoshewa siku 18 ya mwezi ya kumi 2007. Chumba kiliona kama kuko sababu kabisa za kuamini kama Germain Katanga, akiwa kiongozi mkubwa wa FRPI alifanya kazi ya lazima mu kupanga na kufanya, siku 24 za mwezi ya pili 2003 wala karibu ya hii tarehe, shambulio bila kuchagua, ya kijiji ya Bogoro, mu Ituri.

Tena Chumba kiliona kama kuko sababu kabisa za kuamini kama, wakati ya shambulio na kisha shambulio ya kijiji ya Bogoro, yenye ilielekea sana sana raia wa kabila ya Bahema, hizi maenfraksyo za kabambi zilifanyika : mauaji ya karibu raia 200, kuumiza kabisa na kutesa raia; kufunga batu, kuogopesha batu na silaha na kufungia raia mu nyumba yenye inayala maiti; uporaji; kufanya banamuke na batoto banamuke mingi batumwa ba ngono; na batoto ba myaka chini ya 15 kufanya kabisa kuile mapigano.

Chumba kiliona tena kama kuko sababu kabisa za kuamini kama Germain Katanga na biongozi bengine ya FRPI et na ba *Front nationaliste et intégrationniste (FNI)* balifanya pamoya mupango ya bote ya kushambulia kijiji ya Bogoro.

Chumba kinasema kama  kuko sababu kabisa za kuamini kama shambulio ya Bogoro ilifanyika mu hali ya vita mu Ituri na kama ilifanyiwa na FRPI pamoya na FNI mu ya shabulio yenye kupangwa na yayote yenye, kati ya mwezi ya kwanza na karibu mwezi ya tatu 2003, ilielekea raia wa mu fasi zimoya za mtaa ya Ituri, sana sana wa kabila ya Bahema.

**Mashtaka**

Manda ya kukamata Germain Katanga inataya mashtaka kenda, yenye kuangalia  dhima yake ya pekee ya jinai kufuatana na mistari a) na b) za kifungu 25-3 ya Mkataba ya Roma :

- mashtaka tatu ya jinai dhidi ya utu : mauaji (kifungu 7-1-a), matendo ya kinyama (kifungu 7-1-k) na utumwa wa kingono (kifungu 7-1-g) ;
- mashtaka sita ya jinai za vitani : mauaji ya kukusudia (kifungu 8-2-a-i wala 8-2-c-i), matendo ya kinyama (kifungu 8-2-a-ii) wala matendo ya kikatili (kifungu 8-2-c-i), kuingiza kabisa batoto ba miaka chini ya 15  mu mapigano (kifungu 8-2-b-xxvi wala 8-2-e-vii), utumwa wa kingono (kifungu 8-2-b-xxii wala 8-2-e-vi), kushambulia kumakusudi raia wala rai benye habako kabisa mu mapigano (kifungu 8-2-b-i wala 8-2-e-i), na uporaji ya mgini wala ya kijiji, ata kama imeshambuliwa (kifungu 8-2-b-xvi wala 8-2-e-v).

**Byenye Grefyé alisema**

Bw. Bruno Cathala, Grefyé wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai anafurahi na kitendo ya serikali ya Kongo. Alisema : « Bakubwa ya serikali ya Kongo balitumika na Mahakama kufuatana na Mkataba, wakati balifanya byenye manda ya kukamata inaomba na bakapana Germain Katanga ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai».

**Ukumbusho ya hali ya maneno**

Germain Katanga njo mutu wa pili kufungwa na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Siku 17 za mwezi ya tatu 2006 pale Kinshasa, Thomas Lubanga Dyilo, akiwa ni Mkongomani na mwenye kuzaniwa kuwa muundaji tena kiongozi wa *Union des patriotes congolais (UPC)*, alikamatiwaka na kupelekewa ku Mahakama. Hali mu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni moya mu hali ine zenye biro ya Pokirere wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai iko inafanya ndani ankete.

Hali zingine tatu ni : hali mu Uganda, mwenye manda ine za kukamata viongozi wa  *Armée de résistance du Seigneur*  zilifanyiwa; hali  ya kule Darfour (Soudan), mwenye manda za kukamata Ahmad Muhammad Harun, waziri wa zamani wa mambo ya ndani na hii masiku waziri wa mambo ya kiutu wa serikali ya Soudan, na Ali Muhammad Ali Abd-Al-Rahman (alias « Ali Kushayb »), kiongozi wa banamgambo /Janjaouid ; na hali mu Afrika ya kati.

**Manda ya kukamata Germain Katanga**
ICC-01/04-01/07-1 – ya asili :   Kifaransa I  Kingereza
ICC-01/04-01/07-Anx1 – Nyongezo : Kifaransa

**Kartasi ya habari zenye kuangalia masambo**
ICC-PIDS-CIS-DRC2-01-001/07 - Kingereza  |  Kifaransa

**Ginsi masambo inaendeka kiisha kukamata mwenye kuzaniwa kama alifanya makosa na kumupana ku Mahakama**

ICC-PIDS-PRI-1/07 - Kingereza | Kifaransa

**Munyoro ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai**
ICC-PIDS-PRI-02/07 - Kingereza | Kifaransa

**Habari za lazima**

Mukutano na bapasha habari

Prokirere msaidizi, Fatou Bensouda, na Grefyé, M. Bruno Cathala, batafanya mukusanyo na bapasha habari ku makao makuu ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai pale La Haye siku ya tano tarehe 19 ya mwezi ya kumi na saa saba na nusu.

Bapasha habari habalazimishwe kusema kama batakuwa pale.

---

Juu ya habari zaidi, ni muzuri kupata Bibi Sonia Robla, mkuu wa Tawi la habari na hifadhi ya hati. Telefone : +31 (0)70 515-8089 wala telefone ya kumukono +31 (0)6 46 44 87 26 ; e-mail : sonia.robla@icc-cpi.int

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo : Paul Madidi, afisa wa habari na kuelimisha umma uwandani. Telefone :+243 99 801 1403 wala e-mail : paul.madidi@icc-cpi.int